# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**PRECIOUS BLOOD HIGH SCHOOL**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 1**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

**PRECIOUS BLOOD KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016**
**102/1**
**KARATASI YA 1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

---

1. **SWALI LA LAZIMA**
   **SURA**

(i) Kichwa / Anwani ya ripoti.

- Ripoti ni ya nini, nani, nani aliteua jopo na mwaka.

(ii) Utangulizi

- Nani alitaka ripoti iandikwe.
- Muda waliopewa
- Tatizo lenyewe
- Wanajopo na vyeo vyao.

(iii) Mbinu za uchunguzi
- Mfano matumizi ya hojaji, mahojiano n.k.

(iv) Matokeo ya uchunguzi

- Ukabila
- Dini
- Umaskini
- Ukosefu wa ajira
- Misimamo tofauti ya kisiasa

- Mifumo tofauti ya utawala.
- Ugavi wa raslimali za nchi.
- Makundi haramu.
- Ukimbizi
- Uhasama wa kiukoo
- Kisasi
- Tamaa ya mali na mamlaka.
- Ufisadi. Tanbihi: mwanafunzi azingatie angaa hoja nane.

(v) <u>Hitimisho</u>
Tanbihi – Hitimisho liwe fupi na lioane na matokeo ya uchunguzi. (iwe aya moja)

(vi) <u>Mapendekezo</u>

- Huandikwa kwa kuorodheshwa kwa nambari.
- Yatoe suluhisho ama hatua za kuchukuliwa ili kudhibiti ama kusuluhisha tatizo la utovu wa usalama.

<u>Mifano</u>
(i) Serikali iwahamasishe wananchi umuhimu wa kuishi pamoja kwa amani.
(ii) Sheria iundwe ya kuwaadhibu wahalifu.
(iii) Mtazamo wa nyumba kumi utiliwe maanani.
(iv) Ugavi wa raslimali za nchi usawasishwe.
(v) Nafasi za ajira ziongezwe.
(vi) Idara ya elimu iongeze katika mtaala wa masomo somo la umuhimu wa utangamano wa wananchi.
Mwalimu atathmini hoja zozote zingine zinazofaa.

(vii) <u>Mwisho</u>
- Jina la mwandishi na sahihi
- Cheo
- Tarehe

2. <u>Madhara ya teknolojia ya kisasa</u>

(i) Uraibu

(ii) Uzembe kazini

(iii) Ubunifu kudorora

(iv) Utangamano

(v) Upweke

(vi) Mkengeuko (km. mavazi)

(vii) Matumizi ya dawa za kulevya.

(viii) Uzinzi

(ix) Ajali barabara kuongezeka.

<u>Faida</u>

(i) Hurahisisha mawasiliano.

(ii) Utafiti kupitia mtandao (elimu)

(iii) Upanuzi wa biashara

(iv) Usafiri kuimarika.

<u>Tanbihi</u>

(i) Mwanafunzi azingatie pande zote mbili, asipofanya hivyo aadhibiwe kwa kutolewa alama nne.

(ii) Mwanafunzi atoe msimamo wake.

3. <u>Methal</u>

- Mtahiniwa asimulie kuhusu mhusika ambaye maishani mwake alikuwa kipenzi cha kila mtu kwa wema wake.

- Aonyeshe mema aliyowatendea watu wengine kisha atumie sifa hizo kuonyesha jinsi hata baada ya kufa jina lake bado linaishi vinywani vya watu.  Akumbukwe kwa pengo aliloacha.

4. <u>Mdokezo</u>

- Mwanafunzi atamatishe insha yake kwa maneno aliyopewa.  Akiongeza mengine atuzwe alama ya 02.